Mwenyewe

Harmonize

Tisin na nne march fifteen
Begin of my world
Nilipozaliwa nikadondoka chini
Hakukua na kitanda kwa word
Basi mgongo wa mama nikaufanya godoro
Na kilichonikusa mihogo na viporo
Nilipolekwa shule ila bado nikawa mtoro
Kingereza nlichokalili labda tomorrow ama today
Zikafika time ya kubalehe
Nikayajua mapenzi nikagundua bila pesa siyawezi
Ni ujinga

Nikadondokea umachinga
Hapakuchi panakucha siku zikasogea
Pruuh mpka darsalaama nikaanza jitegemea
Nyumbani baba na mama wakiniombea
Mwanetu nenda salama na ukipata lejea
Mmh na ukipata
Hapo akili ndo ikaanza kukomaa
Na nikajuta kwann sikusomaa
Jinsi jua la utosi linavyochoma
Na usiku baridi ilanipa homa nusu inuchukue uhai mmmh
Mi nimepitia mengi ndo mana sio mshamba wa helaa
Kwa ajili ya vitu vidogo sigomban na maselaa
We kubali kudharauliwa
Kukataliwa
Kupata majaliwa
Kula kinacholiwa
Mwenyew

Raha jipe mwenyewe
Basi kamata chupa fungua na mimina
Mwenyewe raha jipe mwenyew
Lewa tukuone unavyocheza kichina
Mwenyewe raha jipe mwenyewe
Anaekupenda zaidi ni wewe
Mwenyew raha jipe mwenyewe
Ata anaekujua zaidi ni wewe
Mwenyewe raha jipe mwenyewe

Masikini na wanawe tajiri na mali zake
Hasie na shida nawe mwache aende zake
Husibweteke na ulicho nacho
Pia husiteseke kwa walicho nacho
Ridhiki mafungu saba pengine leo zam ya sita
Kaza moyo epusha roho yakusita
We umezaliwa peke yako
Utakufa peke yako
Na utazikwa peke yako
So usiwaeleze shida zako
Ukizani ndugu zako kumbe wabaya wako
We komaaa

Mwenyewe raha jipe mwenyew
Basi kamata chupa fungua na mimina
Mwenyewe raha jipe mwenyewe
Lewa tukuone unavyocheza kichina

Mwenyewe raha jipe mwenyewe
Anaekupenda zaidi ni wewe
Mwenyew raha jipe mwenyewe
Ata anaekujua zaidi ni wewe
Mwenyewe raha jipe mwenyewe

Sponzor: www.srovnavac.cz - vyberte si pojištění online!